**Learning by Ear 2011 – Road Safety**

**Episode 02 – Overtaking**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Martin Vogl**

**CHARACTERS:**

Onyesho la 1:

- PAMELA (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 30-40)
- PETER (MWANAMME, UMRI WA MIAKA 60-70, Babamkwe wa Pamela)

Onyesho la 2:

- MUUGUZI(MWANAMKE)
- PAMELA (MWANAMKE, UMRI WA MIAKA 30-40)
- NELSON (MVULANA, UMRI WA MIAKA 14)

Intro/Studio/Outro:

- MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)
- GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI (MWANAMUME)

Tah: Mtangazaji anaweza kuwa mwanamume na mtaalamu wa usalama barabarani anaweza kuwa mwanamke

**Intro:**

**1. Beatrice:** Hamjambo, jina langu ni Beatrice na ningependa kuwakaribisha tena kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na sehemu ya pili ya mchezo wa redio kuhusu usalama barabarani. Katika vipindi vyetu vyote kumi tunaiangazia maisha katika familia ya Wanjiru ambayo inashuhudia hatari za ukosefu wa usalama barabarani. Tunazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tufahamu jinsi ya kuimarisha usalama barabarani kwa lengo la kuokoa maisha.

Katika kipindi kilichopita Samuel alikataa kuweka mikanda ya usalama kwenye basi lake inagwa serikali ilikuwa imetangaza kanuni mpya. Basi lake lilihusika kwenye ajali mbaya; abiria wawili walifariki na wengine watatu, akiwemo mwanawe Nelson, walijeruhiwa vibaya. Lau wote wangekuwa wamejifunga mikanda ya usalama, pengine wangekuwa salama.

Katika kipindi hiki babu yake Nelson, Peter, anampeleka Pamela, mamake Nelson, hospitali kumtembelea mwanawe. Ingawa mjukuu wake amejeruhiwa na yuko hospitalini, Peter anaendesha gari bila kuwa mwangalifu.

**Scene One: in the taxi**

| | |
|---|---|
| **2. SFX Atmo:** | **driving along inside a car** |
| **3. PAMELA:** | Ninaumia kila nikimfikiria Nelson na ajali aliyoipata. Watu wawili walifariki… Najua Nelson alijeruhiwa shingo, lakini pengine angekuwa miongoni mwa waliofariki. Tena babake ndiye aliyekuwa akiendesha hilo gari. Unadhani atadumu na fikra gani? |
| **4. PETER:** | Hali itakuwa nguvu hasa iwapo polisi hawatamfungulia Samuel mashta ka. Pamela, tuoombe Nelson ajaliwe kupona haraka iwezekanvyo na kwamba hatakuwa na matatizo mengine yatakayotugharimu fedha zaidi. |
| **5. PAMELA:** | Baba, ndio hao madereva wa jiji hili... Barabara zenyewe ni mbaya… lakini madereva wanaonekana kama kwamba hawajali maisha yao. Wanahatarisha na maisha ya wengine. |
| **6. PETER:** | Siku hizi hakuna anayefunzwa kuzingatia sheria za barabarani. Nilipokuwa mdogo ilibidi mtu kujitahidi vilivyo ili apite mtihani wa kuendesha gari. Siku hizi ni kama kwamba kwa kutumia fedha unaweza kupata utakacho. Na pia magari makubwa yanaonekana kama kwamba ndo yenye haki zaidi barabarani. Kazi kuwatatiza madereva wengine... |
| **7. SFX:** | **sudden sound of horn** |

**8. PAMELA:** **shrieking**

**9. SFX:** **car bumping over dirt and stones, then stalling**

**10. PETER:** Kuna nini ! Uko sawa?

**11. PAMELA:** **(shocked)** Mungu wangu, lile gari limekuja kwenye upande wetu - lau usingeliepuka tungegongana nalo. Huyo dereva amekuwa na nini?

**12. PETER:** Moyo wanienda mbio. Lakini nadhani gari letu liko sawa.

**13. SFX:** **starts the engine**

**14. PETER:** Tuendelee na safari, Pamela?

**15. PAMELA:** Tuombe tuwasili salama twendako. Maana hizi barabara zinatisha. Ulikuwa ukisema kuhusu magari makubwa yalivyo barabarani na waona yaliyotukia. Jamaa ametupita ghafla bin vuu bila kufikiri kwamba tunaweza kumgonga.

**16. SFX:** **car moves off back onto the road**

**17. PETER:** Twende zetu. Tusije kuchelewa tukafika baada ya saa saba, ambao ndo wakati wa kuwatembelea wagonjwa.

**18. SFX:** **sound of car accelerating**

**19. PAMELA:** Naam. Nafuu tumeondoka kwenye barabara kuu sasa. Barabara hizi ndogo zina upepo mwingi lakini hazina magari mengi. Isipokuwa malori haya… tutaendelea kubaki nyuma ya lori hili mpaka mwisho wa mlima?

**20. PETER:** Hapa, Pamela, hatuwezi! Nitajaribu kulipita.

**21. PAMELA:** Lakini, unaona magari yanayokuja mbele yako, ba?

**22. PETER:** Aaa hapana, lakini nadhani hakuna tatizo.

**23. SFX:** **sound of horn as a car goes speeding by**

**24. PETER:** Looo, nusura tugongane! Acha nijaribu tena.

**25. SFX:** **car accelerates and overtakes**

**26. PAMELA:** **(nervous)** Baba, hatufai kupita magari hivi tunvayoyapita. Kuna mlolongo mrefu wa magari na barabara yenyewe ina upepo mkali na inatatiza. Tena tunapanda mlima. Bora tuwe wastahamilivu mpaka tufike mwisho wa mlima. Bora tufike hospitali kuchelewa kuliko kuangamia hapa barabarani.

**27. PETER:** Hatuwezi tu kusubiri nyuma ya malori haya. Tazama. Watu wengine wanapita- usijali.

**28. PAMELA:** Baba, kama huoni mbele… tafadhali usijihatarishe!

**29. PETER:** Nishakwambia usijali, Pamela. Kila mtu anafanya hivyo. Usiwe na wasiwasi!

**30. SFX:** **sound of horn as a car goes speeding by**

**31. PAMELA:** Baba, waona tena! Gari lako halina hata kasi ya kutosha… Usijaribu tena kuyapita magari... Nimesema usijaribu.

**32. SFX:** **car accelerating**

**33. PAMELA:** Babu tahadhari, lori lile linatokeza barabarani pia...

**34. SFX:** **screech of brakes and crash, the car rolls over**

**<u>Scene Two: Hospital</u>**

**35. SFX Atmo:** **inside a hospital room, people passing by in corridors**

**36. NURSE:** Pamela, unaweza kuchezesha vidole vyako… Pamela jaribu kuchezesha vidole vyako.., Unanisikia Pamela?

**37. PAMELA:** Ahhhh ahhh, ahhhh, naumwa na kichwa...Niko wapi?

**38. NURSE:** Uko hospitalini Pamela, na mimi ni muuguzi wako. Daktari atafika hivi punde. Umeletwa hapa baada ya gari ulilokuwemo kupinduka. Tunadhani huenda ukawa umeumia mgongo ndiposa ninakwambia uchezeshe vidole. Tafadhali fanya hivyo!

**39. PAMELA:** Nadhani. Ninaweza kufanya hivyo.

**40. NURSE:** Una bahati. Hujavunjika mgongo. Tunakuongezea maji ya dawa ya kupunguza maumivu- ulipokuja hapa ulikuwa umepoteza fahamu.

**41. PAMELA:** Na vipi hali ya Peter? Na mwanangu, Nelson? Tulikuwa tukielekea hospitali kumuona mwanangu

**42. NURSE:** Hawana neno. Mwanao alikuja kukuona. Alikuwa katika wadi ya juu lakini amesharuhusiwa kurejea nyumbani. Anasubiri nje pamoja na babu yake. Una bahati sana. Gari lenu halitazamiki lilivyopondeka.

**43. PAMELA:** Hilo gari ni teksi na ndo biashara afanyayo baba mkwe wangu. Atajipatia fedha vipi? Mume wangu naye nusura apoteze basi lake kwa ajali iliyotukia jana... Askari polisi wanahoji pia.

**44. NURSE:** Labda sasa wataanza kuendesha magari kwa uangalifu zaidi … Idadi ya watu wanaoletwa hapa hospitali kwa ajali za magari haihisabiki. Wengine hutoka hapa wakiwa hai na wengi maiti. Ninyi mna bahati sana.

**45. SFX:** **DOOR OPENING**

**46. NELSON:** Mama!

**47. PAMELA**: Nelson! Nelson (breaking down, sobbing). Vipi hali? Njoo hapa, u mzima?

**48. SFX**: **FOOTSTEPS MOVE TO THE BED; PAMELA KISSES NELSON**

**49. NELSON:** Nadhani...na wewe je? Ninachanganyikiwa na mambo yanayotokea. Kwani tumekumbwa na nini, mama? Mbona tunakabiliwa na hizi ajali mbaya mbaya? Naye baba yuko wapi? Mbona hajaja kunitembelea?

**50. PAMELA:** Babako ameshtuka, Nelson. Anajilaumu kwa mambo yaliyotendeka. Anahojiwa na askari polisi na hatujui nini watakachoamua kufanya. Mara nitakaporuhusiwa kuondoka hospitalini tutakwenda nyumbani pamoja. Tunahitaji muda wa kukaa na kuyaangaza haya mambo pamoja. Mbali na hospitalini na barabarani.

**END OF SCENE TWO**

**SHORT MUSIC**

**51. BEATRICE:** Naam, kama mlivyosikia katika kipindi chetu cha pili cha mchezo wa redio kuhusu usalama barabarani, mtu mwengine wa familia ya wanjiru amejipata hospitalini. Hapa studioni niko pamoja na George, mtaalamu wetu wa usalama barabarani. Karibu, George.

**52. GEORGE:** Asante.

**53. BEATRICE:** George, umesikiza kipindi cha pili. Na tena, majeruhi ni abiria aliyekuwa akimrai dereva kuendesha gari kwa uangalifu kabla ya hiyo ajali kutokea. Inaonekana kana kwamba abiria hana uwezo wa kujihakikishia usalama wake barabarani.

**54. GEORGE:** Inaonekana hivyo.Pamela alikuwa akimuonya Peter kutoendesha gari kwa kasi na asiyapita magari mengine kwa kuwa alikisia kwamba Peter hakuwa na uwezo wa kuona mbele yake. Uamuzi wa Pamela ulikuwa sawa lakini yeye ndiye anayeishia hospitalini.

**55. BEATRICE:** Na kwa nini dereva aliamua kuyapita magari ilhali hakuwa akiona magari yaliyokuwa yakija kutokea upande wa pili? Na mbona hakufuata ushauri wa abiria wake?

**56. GEORGE:** Hili si jambo geni barani Afrika. Madereva si waangalifu, hawawajali wenzao barabarani na wala hawatilii maanani ushauri wa abiria.

**57. BEATRICE:** Mbona Peter alijiamini hatoweza kupatikana na lolote? Kwanini alifikiria kuwa angeyapita magari kwa usalama bila hata kuona mbele?

**58. GEORGE:** Ni wazi alidhani anaendesha gari lililokuwa na kasi kushinda malori. Hakuona sababu ya kusubiri nyuma ya malori. Lakini iwapo unaendesha gari kwenye barabara yenye kona nyingi ambapo ni vigumu kuyaona magari yanayokuja, si vizuri kujaribu kuyapita magari yaliyo mbele yako. Kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha yako na ya abiria wako.

**59. BEATRICE:** Na vipi gari linalokuja upande unakoelekea?

**60. GEORGE:** Ajali za magari kugongana ana kwa ana ndo ajali mbaya zaidi hasa magari yanapoendeshwa kwa kasi. Na kwa kawaida mtu anapojaribu kupita gari lililomtangulia huwa anaendesha gari lake kwa kasi. Kwa hivyo mwendo wa kasi na uamuzi huo wa kupita magari ya mbele hasa kwenye kona bila kuona unakokwenda ni mambo mawili hatari yanayoweza kusababisha ajali mbaya.

**61. BEATRICE:** Watu siku hizi wanatenda mambo kwa haraka haraka bila kukaa na kufikiria matokeo yake.

**62. GEORGE:** Ndiyo hivyo. Na barabarani watu wanaoendesha magari kwa pupa ndo walio na uwezekano zaidi wa kusababisha ajali. Hiyo tabia ya kupita magari barabarani ndio sababu moja kuu ya ajali hizi. Ni lazima uhakikishe kwamba unaona vyema unakoelekea kabla ya kutaka kuyapita magari yaliyo mbele yako.

**63. PRESENTER:** Asante sana, George kwa kututembelea hapa studioni.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**<u>OUTRO</u>**

**64. BEATRICE:** Katika kipindi kitakachofuata tumamsikia jinsi Alice Wanjiru, dada yake Nelson, ambaye haendeshi gari wala si abiria, anavyohusika kwenye ajali barabarani. Usikose kujiunga nasi ili tufahamu jinsi madereva wetu wanavyofanya mambo ya hatari barabarani kwenye mchezo mwingine wa redio uliotungwa na Victoria Averill. Iwapo ungetaka kukisikiliza tena kipindi hiki, nenda kwenye ukurasa wetu wa wavuti www.dw.de/lbe. Asante sana kwa kujiunga nasi na hakikisha usalama barabarani!